

## **MSTAHIKI MEYA, MWENYEKITI WA CCM NA WAHESHIWIWA MADIWANI WAPONGEZA UKUSANYAJI WA MAPATO YA NDANI MANISPAA YA MOROGORO**

Kikao cha Mkutano wa Kawaida wa Baraza la Waheshimiwa Madiwani wa Manispaa ya Morogoro kimefanyika jana tarehe 03.08.2023 katika Ukumbi wa Mikutano wa Manispaa hiyo ambapo Mstahiki Meya wa Manispaa, Mheshimiwa Pascal Mwendishule Kihanga, Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Morogoro Mheshimiwa Shukuru na Waheshimiwa Madiwani wa Manispaa wamempongeza Mkurugenzi wa Manispaa hiyo pamoja na timu yake ya wataalamu kwa kufanikiwa kukusanya Mapato ya Ndani ya Manispaa kwa asilimia 109 ambapo jumla ya shilingi bilioni 13 zilikusanywa katika mwaka wa fedha 2022/2023 uliofungwa mwezi Juni 2023.



Katika salamu zake za ufunguzi wa kikao hicho, Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, Mheshimiwa Pascal Kihanga amesema, kwa kuwa Manispaa imefanya vizuri sana kimapato katika mwaka wa fedha uliomalizika na sasa kiuchumi iko vizuri hii inadhihirsha kiu ya uongozi na Menejimenti nzima ya Manispaa kuwa Jiji.



Amemtaka Mkurugenzi wa Manispaa kuangalia mkakati wa kuwa jiji unaanzia wapi ili Manispaa iweze kuufanya huku akikisitiza kuendelea kuongeza ubunifu zaidi katika ukusanyaji wa mapato ya Manispaa ili mwishoni mwa mwaka huu kuwepo na ongezeko zaidi la makusanyo ya mapato.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Morogoro, Mheshimiwa Fikiri Juma, amepongeza utendaji wa Mkurugenzi, timu ya Wataalamu na Waheshimiwa Madiwani katika miradi mbalimbali ya maendeleo kwa fedha kutoka serikali Kuu na Mapato ya Ndani ya Manispaa.



"Mmeshughulika vizuri na ujenzi katika sekta ya Elimu Sekondari, kupitia fedha za BOOST pia tumeona mlivyotekeleza kwa wakati miradi hiyo na hii ni kwa sababu kila mmoja wenu aliwajibika ipasavyo kwenye eneo lake. Wito wangu tusibaki pale tulipoishia, endeleeni kubuni vyanzo vingine vya mapato na ushirikiano huu katika kazi uendelee ili tufikie mafanikio makubwa" alisema Mheshimiwa Juma.

Kwa upande wao Waheshimiwa Madiwani, wamepongeza matumizi sahihi ya fedha za miradi ya maendeleo na wamemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa fedha hizo ambazo zimesaidia kujenga Zahanati nyingi, vyumba vya madarasa, mabweni, majengo ya utawala na matundu ya vyoo mashuleni.

Aidha, Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Ndugu Ally Machelo amesema pongezi hizo zinamfanya yeye pamoja na timu yake ya wataalamu waongeze juhudi zaidi katika utumishi wao na amebainisha miradi mbalimbali ambayo inaendelea kutekelezwa hivi sasa na Manispaa.

"Katika mwaka huu wa fedha tunapanga kukarabati ama kuzijenga upya shule kongwe zote, tunajenga bwalo kubwa katika kambi ya wazee ya Fungafunga ili kuwafanya wazee hao wawe na kitega uchumi na mahali pazuri pa kulia chakula, mwaka huu pia tutajenga jengo la upasuaji katika Vituo vya Afya Sabasaba na Mafiga, robo hii ya kwanza tutakamilisha ujenzi wa Zahanati zetu sita na kuhakikisha zinaanza kufanya kazi na katika robo ya pili ya mwaka huu tutakamilisha ujenzi wa kituo cha Afya Tungi" alieleza Machelo.



Mwisho, Mkurugenzi Machela ameufahamisha umma wa Manispaa ya Morogoro kuhusu mapokezi mashine ya kutoa dawa ya usingizi katika Kituo cha Afya SabaSaba.

“Tumepokea kutoka MSD mashine ya kutoa dawa ya usingizi (Anaesthesia Mchine) kwa ajili ya upasuaji. Tunatazamia ndani ya mwezi huu tutakamilisha ufungaji wa mashine hiyo na madaktari waliopo kwenye kituo chetu cha afya cha SabaSaba watakuwa wakiendelea kufanya upasuaji kituoni pale. Akina mama pia wataweza kufanyiwa upasuaji wa uzazi na huduma hii ndio kipaumbele kwetu, na hii itapunguza msongamano katika Hospitali ya Rufaa Morogoro” alifafanua Machela.



**MWISHO**

